sekretarieti ya maadili

# Jarida la MAADILI

Toleo la 04: Januari- Machi 2024

www.matadili.go.tz

DIRA:UADILIFU KWA VIONGOZI WA UMMA

## MHE. DKT. SAMIA AFANYA MABADILIKO YA ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mabadiliko katika orodha ya Viongozi wa Umma hivi karibuni. Mabadiliko hayo yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 kinachompa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kuongeza, kufuta au kuboresha orodha ya Viongozi wanaotambuliwa kwa mujibu wa Sheria.

Mabadiliko hayo yalitangazwa katika gazeti la Serikali Na. 857 la tarehe 24.11.2023.

**Inaendelea ukurasa wa 5...**




## SEKRETARIETI YA MAADILI YAANZA KUPOKEA MATAMKO KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE DECRELATION SYSTERM - ODS).

**Scan kusoma Jarida Kidijitali**

"Mfumo wa ujazaji Tamko kwa njia ya Mtandao (ODS) ni Mfumo mpya ambao unamuwezesha Kiongozi wa Umma kujaza na kuwasilisha Tamko la Raslimali na Madeni pamoja na Ahadi ya Uadilifu kwa njia ya Mtandao".

**Inaendelea ukurasa wa 9..**

## MAJALIWA: TUUNGANISHE NGUVU KUJENGA KIZAZI CHENYE MISINGI YA MAADILI

"Maadili yanajengwa kuanzia kwenye taasisi na taasisi ya kwanza ya ujenzi wa maadili kuwa ni familia, Taasisi ya pili ni shule ambayo inawajibika kuweka mifumo ya kuendeleza kile kilichopatikana nyumbani."

**Inaendelea ukurasa wa 7..**

# YALIYOMO

TAHARIRI ........................................................ 3

MAMLAKA NA MAJUKUMU YA TAASISI ........................................................ 4

SAMIA AFANYA MADADILIKO YA ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA........................................ 5-6

TUUNGANISHE NGUVU KUJENGA KIZAZI CHENYE MAADILI ........................................ -8

SEKRETARIETI YA MAADILI YAANZA KUPOKEA MATAMKO KWA NJIA YA MTANDAO

(ONLINE DECRELATION SYSTERM - ODS)........................................................ 9

HABARI KATIKA PICHA ........................................................ 10

HABARI KATIKA PICHA........................................................ 11

HABARI KATIKA PICHA........................................................ 12

MAAFISA WA JESHI LA POLISI WAMETAKIWA KUZINGATIA MAADILI ........................................ 13

TUJIKITE KUZUIA RUSHWA BADALA YA KUPAMBANA MADHARA YAKE........................................ 14

HABARI KATIKA PICHA ........................................................ 5

HABARI KATIKA PICHA ........................................................ 16

VIONGOZI WA UMMA WATAKIWA KUJIEPUSHA NA MGONGANO WA MASLAHI ........................... 7

HABARI KATIKA PICHA........................................................ 8

MAWASILIANO YA OFISI........................................................ 19

## DIRA NA DHIMA

### DIRA
Uadilifu kwa Viongozi wa Umma.

### DHIMA
Kuhakikisha utamaduni wa Uadilifu kwa Viongozi wa Umma wote kupitia kukuza na kufuatilia tabia za viongozi wa umma na kusimamia mgongano wa maslahi ili kujenga imani kwa umma katika kukuza maendeleo ya Taifa.

**Scan kusoma Jarida Kidijitali**

# TAHARIRI

## HONGERA MHE. RAIS KWA KUBORESHA ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA

Tarehe 24 Novemba, 2023 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko ya orodha ya viongozi wa umma kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma , sura ya 398 kupitia notisi katika gazeti la Serikali Na. 857 la tarehe 24 Novemba, 2023.

Mabadiliko hayo yameweka pamoja orodha za viongozi wa umma zilizokuwa katika kifungu cha 4 cha Sheria nyongeza ya viongozi wa umma ya mwaka 2005 na 2013, kubadilisha baadhi ya nyadhifa na kuongeza nyadhifa nyingine ambazo hazikuwepo kwenye orodha za awali.

Notisi hiyo, imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398 kinachompa Mhe. Rais mamlaka ya kurekebisha au kufanya mabadiliko katika orodha ya Viongozi wa Umma.

Notisi hiyo, inajulikana kama Notisi ya kubadili orodha ya Viongozi wa Umma katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2023. Lengo lake ni kuongeza wigo wa Viongozi wa Umma wanaowajibika chini ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kurahisisha rejea ya viongozi hao kwa kuwa na orodha moja tu ya viongozi wa umma. Aidha, orodha hiyo inalenga kuongeza uwajibikaji na kuzuia vitendo vya mgongano wa maslahi miongoni mwa watumishi wa umma.



*Kamishna wa Maadili, Mhe. Jaji (Mst.) Sivangilwa Mwangesi*

Gazeti la Serikali Na. 857 la Novemba 24, 2023 linafuta notisi Na. 209 ya mwaka 2005 na notisi Na. 260 ya mwaka 2013.

Itakumbukwa kuwa kabla ya mabadiliko ya orodha hiyo, kulikuwa na baadhi ya watumishi wa umma waliokuwa na nyadhifa nyeti na mamlaka makubwa katika utumishi wao wa umma, lakini hawakutambuliwa au kuwajibika kama Viongozi wa Umma na Sekretarieti ya Maadili haikuwa na mamlaka ya kuwasimamia baadhi ya watumishi ambao hawakuwa kwenye orodha ya viongozi wa umma.

Miongoni mwa Viongozi hao ni pamoja na, Wakuu wa Vitengo katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa isipokuwa Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi ambao kabla ya orodha mpya walitambuliwa kama Viongozi wa Umma. Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa na Wilaya na baadhi ya taasisi za umma, Wakuu wa TAKUKURU Mkoa na Wilaya n.k.

Mabadiliko hayo pia yanawahusu baadhi ya watumishi wa umma kwenye Wizara, Idara za Serikali, Taasisi za Umma, Mamlaka za Serikali, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao hapo awali hawakutambuliwa kama Viongozi wa Umma. Nyongeza hiyo ya orodha ya Viongozi wa Umma inajumuisha nyadhifa mpya 26 ambazo hapo awali hazikuwemo katika orodha ya Viongozi na inafanya nyadhifa za viongozi wanaowajibika chini ya Sheria ya Maadili kufikia 62.

Kwa muktadha huo, viongozi wote wanaotambulika kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakiwemo waliojumuishwa hivi karibuni, wanatakiwa kufuata masharti yote yaliyomo kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma tangu tarehe ya tangazo.

Baadhi ya masharti hayo ni pamoja na kufuata Nguzo za msingi za Maadili katika Utumishi wa umma ambazo ni; Uadilifu, Uaminifu, Uwazi, kutunza siri, kuepuka mgongano wa maslahi, Uwajibikaji na kuwa na tabia na mwenendo mwema baada ya kustaafu au kuacha kazi.

Tunampongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuboresha orodha ya Viongozi wa Umma. Pongezi zetu pia tunazitoa kwa wadau wengine wa maadili walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuwezesha mchakato wa kuboresha orodha hii mpya.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inawahimiza viongozi wote nchini kutambua wajibu wao na nafasi zao kisheria, kuhakikisha masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa na kuongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao ili kwa pamoja tuijenge na kuistawisha nchi yetu.

Kwa nafasi hii, tunapenda pia kuwashukuru Viongozi wote wa Umma nchini kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwetu tunapotekeleza majukumu yetu.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendelea kutekeleza wajibu wake wa kisheria wa kusimamia tabia na mwenendo wa Viongozi wote wa Umma nchini bila kutetereka.


### WAJUMBE WA BODI YA UHARIRI

Bw. Honoratus Ishengoma...........Mwenyekiti
Bi. Johanither Barongo................Katibu
Bi. Grace Mariki..........................Mjumbe
Bw. Baraka Mwashambwa............Mjumbe



*Kamishna wa Maadili, Mhe. Jaji (Mst.) Sivangilwa Sikalalilwa Mwangesi akiongoza kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa viongozi mbalimbali walioapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hafla hiyo ilifanyika Ikulu Dar-es-Salaam tarehe 19 Machi, 2023.*

## MAJUKUMU NA KAZI ZA OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina mamlaka na majukumu yafuatayo:-

- Kupokea taarifa za mali na madeni zinazohitajika kutolewa na Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria;
- Kupokea malalamiko na tuhuma kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wanachi;
- Kufanya uchunguzi wa awali wa tuhuma au malalamiko dhidi ya kiongozi yoyote wa umma anayetuhumiwa kuvunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi;
- Kuanzisha na kufanya uchunguzi wowote kuhusu ukiukwaji wa Maadili yaliyotajwa katika Sheria bila kusubiri malalamiko kutoka kwa Wananchi;
- Kuhakiki taarifa za Rasilimali na Madeni zinazotolewa na Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria;
- Kuwaelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na kazi za Sekretarieti;
- Kutunza daftari la Rasilimali , Maslahi na Madeni ya Viongozi wa Umma;
- Kuratibu na kuwezesha shughulli za Baraza la Maadili;
- Kuwasilisha kwa Rais mapendekezo ya Baraza la Maadili kuhusu uchunguzi wa kina wa tuhuma za ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
- Kufanya utafiti juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
- Kumtaka mtu yoyote kufika mbele ya Sekretarieti ya Maadili kwa ajili ya mahojiano ambayo yatasaidia katika uchunguzi wa ukiukwaji wa maadili;
- Kukagua akaunti ya Benki ya Kiongozi yoyote wa Umma kwa idhini ya Mahakama pale ambapo Sekretarieti inata-rajia kufanya uchunguzi dhidi ya kiongozi husika;
- Kumtaka Kiongozi anayetuhumiwa kwa kutoa tamko la uongo la rasilimali zake kuthibitisha au kurekebisha Tam-ko lake;
- Kutoa idhini ya kukagua Daftari la Raslimali, Maslahi na Madeni ya Kiongozi wa Umma kwa Mwananchi aliyekidhi vigezo;
- Kumtaka mtu yoyote kuwasilisha kitabu, nyaraka au nakala iliyothibitishwa au kielelezo chochote ambacho kita-saidia uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa Maadili.



*Mkuu wa kitengo cha huduma za Sheria, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Bi. Emma Gelani akitoa mada kuhusu sheria ya Maadili kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya Habari nchini katika mkutano wa Sekretarieti ya Maadili na wahariri uliofanyika katika ukumbi wa Arnaotoglou Jijini Dar es Salaam tarehe 17 Juni ,2023.*

# MHE. DKT. SAMIA AFANYA MADADILIKO YA ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA

**Inatoka Ukurasa wa 1...**

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mabadiliko katika orodha ya Viongozi wa Umma.

Mabadiliko hayo yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 kinachompa Mhe. Rais mamlaka ya kuongeza, kufuta au kuboresha orodha ya Viongozi wanaotambuliwa kwa mujibu wa Sheria.

Mabadiliko hayo yalitangazwa katika gazeti la Serikali Na. 857 la tarehe 24.11.2023.

Kwa mujibu wa tangazo hilo la Serikali, mabadiliko hayo yanagusa nyadhifa mbalimbali za watumishi wa umma katika Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya umma, Mamlaka za Serikali, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995, viongozi wote wa umma waliotamkwa katika tangazo Na. 857 wanatakiwa kuzingatia misingi yote inayoainishwa chini ya Sheria.

Ifuatayo ni orodha ya viongozi wa Umma kama ilivyotolewa hivi karibuni;

(i) Rais wa Jamhuri ya Muungano;
(ii) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;
(iii) Rais wa Zanzibar;
(iv) Waziri Mkuu;
(v) Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;
(vi) Spika, Naibu Spika na Mbunge;
(vii) Jaji Mkuu, Jaji wa Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu na Hakimu;
(viii) Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya;
(ix) Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serkali;
(x) Balozi Mwakilishi wa Tanzania nchi za Nje;
(xi) Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Tawala wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa Msaidizi na Katibu Tawala wa Wilaya;
(xii) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Nje;
(xiii) Katibu wa Bunge;
(xiv) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi;
(xv) Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi;
(xvi) Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa;
(xvii) Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza;
(xviii) Kamishna Jenerali wa Uhamiaji;
(xix) Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
(xx) Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya;
(xxi) Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa;
(xxii) Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Mkuu wa TAKUKU RU Mkoa na Mkuu wa TAKUKURU Wilaya;
(xxiii) Afisa katika Jeshi la Ulinzi kuanzia cheo cha Kanali;
(xxiv) Afisa katika Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zima moto na Uokoaji kuanzia cheo cha Kamishna Msaidizi;
(xxv) Kamanda wa Polisi Mkoa, Mkuwa Upelelezi Mkoa, Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa, Mkuu wa Polisi Wilaya, Mkuu wa Upelelezi Wilaya na Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya;
(xxvi) Mkuu wa Magereza Mkoa na Mkuu wa Gereza;
(xxvii) Gavana na Naibu Gavana;
(xxviii) Mtendaji Mkuu na Naibu Mtendaji Mkuu katika Taasisi, Idara, Mamlaka, Wakala wa Serikali, Shirika na Kampuni ya Umma;
(xxix) Mwakilishi wa Serikali katika Shirika au Kampuni ambayo Serikali ina Maslahi;
(xxx) Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Diwani;
(xxxi) Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi, Mkurugenzi Msaidizi, Katibu, Naibu Katibu, Katibu Msaidizi na Meneja katika Wizara, Taasisi ya Umma, Idara ya Serikali, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(xxxii) Mkuu wa Idara au Kitengo katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la

**Inaendelea ukurasa wa 6..**




**Scan kusoma Orodha ya Viongozi**

**Inatoka Ukurasa wa 5 ...**

Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(xxxiii) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mjumbe au Kamishna katika Tume;

(xxxiv) Msajili, Mrajisi, Naibu Msajili, Naibu Mrajisi, Msajili Msaidizi, Mrajisi Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(xxxv) Kamishna na Kamishna Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali na Wakala wa Serikali;

(xxxvi) Katibu Binafsi na Naibu Katibu au Katibu Msaidizi Binafsi wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;

(xxxvii) Mshauri wa Rais;

(xxxviii) Msaidizi wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;

(xxxix) Mwandishi wa Habari, Mwandishi wa Habari Msaidizi na Mpiga Picha wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;

(xl) Mratibu, Mratibu Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka na Wakala wa Serikali;

(xli) Mratibu wa Mradi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(xlii) Mnikulu na Naibu Mnikulu;

(xliii) Karani na Naibu Karani wa Baraza la Mawaziri;

(xliv) Msaidizi wa Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza la Mawaziri;

(xlv) Mganga Mkuu na Mfamasia Mkuu wa Serikali, Mganga Mkuu wa Mkoa, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kanda, Mkoa na Wilaya;

(xlvi) Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi na Mkuu wa Hazina Ndogo na Mhakikimali wa Mkoa na Wilaya.

(xlvii) Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Msaidizi;

(xlviii) Msajili Mkuu, Msajili na Naibu Msajili wa Mahakama;



*Kamishna wa Maadili, Mhe. Jaji (Mst) Sivangilwa Mwangesi (hayupo pichani) akiongoza kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa viongozi mbalimbali walioteuliwa, hafla hiyo ilifanyika Ikulu Dar es Salaam tarehe 26 Septemba, 2023.*

(xlix) Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mtendaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu;

(l) Mwandishi Mkuu wa Sheria;

(li) Msajili wa Hazina;

(lii) Mhasibu Mkuu na Mkaguzi wa Ndani Mkuu katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(liii) Makamu Mkuu wa Chuo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mkuu wa Kampasi, Mkuu wa Ndaki, Mkuu wa Kitivo na Mkuu wa Shule katika Chuo Kikuu cha Umma;

(liv) Mkuu wa Chuo, Naibu Mkuu wa Chuo, Mkuu wa Kampasi, Mkuu wa Ndaki na Mkuu wa Kitivo katika Taasisi ya Elimu;

(lv) Mthamini Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba wa Wilaya;

(lvi) Afisa Usalama Mkoa na Wilaya;

(lvii) Mkurugenzi wa Mashtaka, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkuu wa Mashtaka Mkoa na Mwendesha Mashtaka Wilaya;

(lviii) Wakili Mkuu wa Serikali na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali;

(lix) Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu;

(lx) Msuluhishi na Muamuzi katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi;

(lxi) Afisa Madini Mkazi; na

(lxii) Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi katika Bodi ya Wakurugenzi na Bodi ya Wadhamini katika Taasisi ya Umma.".



*Rais wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi mbalimbali pamoja na majaji wa Mhakama ya Rufani na majaji wa Mahakama kuu mara baada ya kuwaapisha majaji hao Ikulu ya Dar es Salaam, Septemba 14, 2023.*

**Scan kusoma Orodha ya Viongozi**

# MAJALIWA: TUUNGANISHE NGUVU KUJENGA KIZAZI CHENYE MISINGI




*Waziri Mkuu wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akihutubia katika maadhimisho ya kilele cha wiki ya Maadili na Haki za Binadamu ambayo yalifanyika jijini Dodoma katika viwanja vya Nyerere Square tarehe 10, Desemba 2023.*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kila tarehe 10 Desemba kuanzia mwaka 2016.

Maadhimisho haya yanatokana na Madhimisho ya kila mwaka ya Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Rushwa ambayo Kimataifa uadhimishwa tarehe 9 Desemba pamoja na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ambayo uadhimishwa kila tarehe 10 Desemba.

Kwa kuwa tarehe 9 Desemba ni siku ya Uhuru na Jamhuri wa nchi yetu, siku ya Maadili huadhimishwa tarehe 10 Desemba. Chimbuko la Siku ya Maadili, ni Siku ya Kimataifa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo huadhimishwa kila tarehe 9 Desemba.

Siku ya Maadili ilianza kuadhimishwa rasmi tangu mwaka 2004 baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuzuia na Kupambana na Rushwa (United Nations Convention Against Corruption – UNCAC). Mkataba huo ulisainiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa mjini Merida, Mexico tarehe 9 Desemba, 2003.

Aidha, kila tarehe 10 Desemba, Tanzania huungana na nchi nyingine Duniani kuadhimisha Siku ya Haki za Binadamu Kimataifa. Chimbuko la Siku ya Haki za Binadamu ni tamko la Haki za Binadamu liililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, tarehe 10 Desemba, 1948 (Universal Declaration of Human Rights - UDHR). Mwaka 2023, Tamko hilo lilitimiza miaka 75.

Kutokana na siku hizo mbili kuadhimishwa tarehe moja, mwaka 2016, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kuunganisha maadhimisho hayo na kuyaita Siku ya Maadili na Haki za Binadamu.

Maadhimisho haya tangu mwaka 2016 yanaratinbiwa na Taasisi Simamizi za masuala ya Utawala Bora na Haki za Binadamu nchini. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais, Ikulu. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Katiba na Sheria, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, Tume ya Utumishi wa Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Katika Maadhimisho ya mwaka 2023, shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho hayo. Shughuli hizo ni pamoja na uzinduzi wa Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu tarehe 3 Desemba, 2023 kwa mbio za Sepesha Rushwa marathoni zilizoanzia na kuhitimishwa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. Mbio hizo ziliwashirikisha wadau kutoka mikoa mbalimbali nchini. Shughuli nyingine ni Jukwaa la Kitaifa la wadau dhidi ya Rushwa, Wiki ya Utoaji Huduma na Siku ya Kilele. Shughuli zote hizi zilifanyika jijini Dodoma. Madhimisho haya pia yalifanyika katika ngazi ya kanda ambapo Kauli Mbiu ya Maadhimisho ilikuwa ni "Zingatia Maadili, Utu, Uhuru na Haki kwa Maende

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ambaye alikuwa Mgeni rasmi wakati wa Kilele cha Maadhimisho hayo alipongeza Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho kwa kuja na kaulimbiu inayowakumbusha Watanzania wajibu wao na kuchagiza masuala ya msingi

Inaendelea ukurasa wa 8..

# MAJALIWA: TUUNGANISHE NGUVU KUJENGA KIZAZI CHENYE MISINGI YA MAADILI

**Inatoka Ukurasa wa 7 ...**

yanayohusu maendeleo endelevu kutokana na ukweli kwamba kizazi huru chenye uadilifu, utu, na kinachozingatia haki ni msingi wa maendeleo ya Taifa lolote.

"Kaulimbiu hii kwa upande mwingine, ni wito kwa kila mmoja wetu, kwa nafasi yake, rika lake na jinsia yake kutekeleza wajibu wake katika ujenzi wa kizazi chenye maadili na hatimaye kujenga jamii yenye ustawi. Pia ni wito kwa sekta ya umma na sekta binafsi kutimiza wajibu wake kuhusu masuala ya maadili, utu, uhuru na haki," alisema.

Kwa mujibu wa Mhe. Majaliwa, maadili yanajengwa kuanzia kwenye taasisi ya msingi na kuitaja taasisi ya kwanza ya ujenzi wa maadili kuwa ni familia.

"Taasisi ya pili ni shule ambayo inawajibika kuweka mifumo ya kuendeleza kile kilichopatikana nyumbani."

Mhe. Majaliwa aliyataja maeneo mengine ya ujenzi wa maadili kuwa ni nyumba za ibada yanapojengwa maadili mema kwa misingi ya kiroho na ushiriki wa jamii nzima kupitia wazee wa ukoo na wazee maarufu katika makuzi ya watoto.

Aidha Mhe. Majaliwa katika hotuba yake aliyoitoa katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma alisema, "hatuna budi wananchi wote kuunganisha nguvu katika ujenzi wa kizazi chenye misingi ya maadili."

"Nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kusimamia na kutekeleza masuala ya haki za binadamu na kuzingatia misingi ya utawala bora katika vipindi vya kabla na baada ya mwaka 1984 ambapo haki za msingi za binadamu ziliingizwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ile ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2010)," alisema.

Wadau mbali mbali wa maadili na haki za binadamu wakiwemo viongozi wa dini, viongozi wa siasa, watumishi wa umma, azaki, mashirika yasiyo ya kiserikali, viongozi na wanachama wa klabu za maadili, washiriki wa maendeleo na wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na mkuu wa Mkoa Mhe. Rosemary Senyemule walishiriki maadhimisho hayo.

Mhe. Majaliwa aliwapongeza kwa ushiriki wao na kusema, "Ushiriki wenu ni ishara ya dhamira ya pamoja ya Watanzania ya kuhakikisha kuwa uadilifu unajengwa, rushwa inadhibitiwa na haki za binadamu zinalindwa ipasavyo."

Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu mwaka 2023, yalienda sambamba na uzinduzi wa Awamu ya Nne ya Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa (National Anti- Corruption Strategy and Action Plan – IV).



*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 10, Desemba 2023, ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa.*

# SEKRETARIETI YA MAADILI YAANZA KUPOKEA MATAMKO KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE DECRELATION SYSTERM - ODS).




*Bw. Waziri Kipacha, Katibu ukuzaji Maadili (katikati) akiongea na waandishi wa Habari tarehe 21 Desemba 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Sekretarieti ya maadili jijini Dodoma kuhusu urejeshaji wa matamko ya Viongozi Kulia kwake ni Bi. Sigolwike Mkamati, Katibu Msaidizi Idara ya usimamizi wa Maadili na kushoto ni Bw. Stanslaus Mwita, aliyekuwa Mkuu wa kitengo cha TEHAMA.*

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Idara ya Serikali inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kwa lengo la kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Na. 13 ya mwaka 1995 yanazingatiwa ipasavyo na Viongozi wote wa Umma.

Kwa Mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, jukumu kubwa la Sekretarieti ya Maadili ni kukuza na kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma nchini ili kuhakikisha kwamba Viongozi wa Umma wanakuwa na tabia na mwenendo wa kimaadili.

Pamoja na jukumu hilo, Ibara ya 132 (5) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema, "Sekretarieti ya Maadili itawataka watu wanaoshika nafasi fulani za madaraka kutoa mara kwa mara maelezo rasmi kuhusu mapato, rasilimali na madeni yao."

Kwa msingi huo wa Kikatiba, Sekretarieti ya Maadili imekuwa kila ifikapo tarehe 31 Desemba ikipokea matamko ya rasilimali na madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma.

Matamko hayo tangu kuanzishwa kwa Taasisi yamekuwa yakitolewa katika utaratibu wa nakala ngumu (hardcopy).

Utaratibu huu umekuwa ukiwasababishia usumbufu mkubwa viongozi kwa kulazimika kusafiri hadi zilipo ofisi za Sekretarieti ya Maadili kuwasilisha matamko yao au kutuma kwa posta kwa njia ya 'registered mail' ikiwemo 'EMS.' Kutokana na hali hiyo na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeamua kuwaondolea Viongozi usumbufu waliokuwa wakiupata kwa kuanzisha Mfumo wa ujazaji na utoaji wa matamko kwa njia ya mtandao 'Online Declaration System – ODS.'

Mfumo wa ujazaji Tamko kwa njia ya Mtandao (ODS) ni Mfumo mpya ambao unamuwezesha Kiongozi wa Umma kujaza na kuwasilisha Tamko la Raslimali na Madeni pamoja na Ahadi ya Uadilifu kwa njia ya Mtandao.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni jijini Dodoma kuhusu ODS, Bw. Waziri Kipacha, Katibu Ukuzaji Maadili alisema, "Mfumo huu wa ujazaji fomu za tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao utawawezesha Viongozi kujaza matamko yao kwa urahisi na kwa usahihi zaidi popote pale watakapokuwa iwe ndani au nje ya nchi."

Viongozi wa Umma wanaweza kuingia katika mfumo kwa kutumia anuani ya https://ods.maadili.go.tz au kupitia tovuti ya Taasisi yenye anuani ya www.maadili.go.tz na kubonyeza kitufe chenye neno 'ODS'. Hapo kiongozi ataingia moja kwa moja kuanza kujaza na kutuma Tamko bila wasiwasi.

Kwa mujibu wa Katibu Ukuzaji Maadili, ODS itamsaidia kiongozi kutosafiri mwendo mrefu na kumpunguzia gharama za kupakua fomu za tamko kuzijaza na kuzituma kwa njia ya posta ambapo hutumia fedha na muda ili kuzifikia katika ofisi za Sekretarieti ya Maadili.

Bw. Kipacha alifafanua zaidi kuwa, Mfumo huu pia utaondoa uwezekano wa kupokea Matamko kutoka kwa watumishi ambao sio Viongozi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995. Kiongozi atakayejaza Tamko atakuwa ametengenezewa akaunti na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hivyo, matamko yatakayopokelewa yatakuwa ya Viongozi wanaowajibika na Sheria ya Maadili na si vinginevyo".

Aidha, baada ya kuanzisha mfumo huu, Viongozi wote wanaoteuliwa au kupandishwa vyeo na kuwajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na wanaokoma uongozi kwa sababu yoyote ile wanapaswa kutuma taarifa zao Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupitia anuani ya barua pepe "helpdesk@maadili.go.tz" ili waweze kutengenezewa akaunti za kuingilia katika mfumo huo.

Kwa upande wake Bw. Stanslaus Mwita, Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) amefafanua kuwa, ujenzi wa Mfumo huu umezingatia usalama na usiri wa taarifa za viongozi.
"Kiongozi akisha ingiza nywila, juu mkono wake wa kulia kuna neno mwongozo, alibonyeze, litatokea tena mkono wa kushoto abonyeze tena na kupakua. Hapo atapata nakala ngumu na picha jongefu (video) vitakavyomsaidia kujaza tamko kwa usahihi," alisema.

ODS imeanza kutumika rasmi mwezi Desemba, 2023 ambapo kupitia mfumo huu, Kiongozi anaweza kujaza Tamko kutokea mahali popote alipo ambapo kuna mtandao wa internet. Njia hii ni rahisi na ya haraka kwa Kiongozi kuweza kujaza Tamko ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Njia hii ni ya uhakika na inaleta nafuu ya gharama pamoja na kuokoa muda kwa Kiongozi na Sekretarieti ya Maadili.

## HABARI PICHA



*Bi. Jasmini Awadhi, Katibu Msaidizi Kanda ya Kati, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Kati Dodoma, akiongea na wanachama wa Klabu ya Maadili ambao ni wanafunzi wa shule ya msingi Makulu jijini Dodoma kuhusu umhimu wa utunzaji wa mazingira kabla ya kuanza zoezi la upandaji miti shuleni hapo, pembeni yake ni Bw. Amon Sembiga Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Makulu, tarehe 19 Januari 2024.*



*Bi. Ester George Afisa Tehama Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, akitoa mafunzo ya mfumo wa ujazaji tamko kwa njia ya mtandao (ODS) kwa baadhi ya waheshimiwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ODS ni mfumo mpya ambao unamuwezesha kiongozi wa Umma kujaza na kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni Pamoja na Ahadi ya Uadilifu kwa njia ya mtandao, mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Bunge kuanzia tarehe 8 hadi 10 Novemba 2023.*


## HABARI PICHA



*Afisa Maadili kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Bi. Modesta Mtui akiongoza kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi mbalimbali kutoka Benki kuu ya Tanzania (BOT). Hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Ofisi za Benki kuu ya Tanzania Dodoma tarehe 24 Novemba,2023*




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb) akitoa neno la utangulizi katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu. Hafla hiyo ilifanyika katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma tarehe 10 Disemba,2023*


VYOTE HIVI NIMEVIPATA KWA NJIA HALALI
NA NITAVITAJA KATIKA TAMKO LA RASILIMALI NA MADENI


UJENZI WA MADARASA
NIMEKUJA KUKAGUA MATUMIZI SAHIHI YA FEDHA ZA UJENZI
SAWA MKUU



*Katibu Msaidizi, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Viongozi wa Umma Kanda Maalum Dar es Salaam , Bi. Elizabeth Komba (Hayupo pichani) akiongoza kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi Zanzibar, hafla iyo ilifanyika ukumbi wa Chuo cha Polisi Zanzibar tarehe 29 Novemba 2023*

## MAAFISA WAANDAMIZI WA JESHI LA POLISI WAMETAKIWA KUZINGATIA MAADILI:

Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi Zanzibar wametakiwa kufanyakazi kwa Uadilifu na weledi mkubwa wanapotekeleza Majukumu yao kwa dhamana waliyopewa ili kujenga imani kwa wananchi wanaowaongoza pamoja na Serikali kwa ujumla.

Kauli hiyo imetolewa na Kamishna wa Polisi Zanzibar CP Hamad Khamis Hamad alipokuwa akifungua mafunzo ya Maadili kwa Maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi yaliyofanyika katika Chuo cha Polisi Zanzibar tarehe 29 Novemba 2023.

Kamishna Hamad katika hotuba yake ameeleza kuwa, jamii ikikosa imani na jeshi la polisi yaweza kupelekea amani ya Nchi kutoweka na kusababisha migogoro nchini.

Aidha Kamishna Hamad alibainisha kuwa "kusimamia sharia bila uadilifu yaweza kusababisha machafuko katika nchi yetu" alisema.

Kamishana huyo pia alifafanua kuwa matendo yanayofanywa na jeshi la polisi katika kusimamia sheria ni lazima yawe ya mfano katika jamii na Serikali kwa ujmla.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Katibu Msaidizi Kanda Maalumu Bi, Elizabeth Komba amewataka Maafisa hao kuwa mstari wa mbele katika kusimamia Maadili katika kutekeleza Majukumu yao kwa Uadilifu na weledi wa kiwango cha juu.

Bi Komba pia amewataka Maafisa hao kuyaishi yote yatakayofundishwa katika mafunzo hayo kupitia mada mbalimbali zilizoandaliwa katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku.

Amefafanua kuwa miongoni mwa mada zitakazojadiliwa ni pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mgongano wa Maslahi, Ahadi ya Uadilifu pamoja na Tamko la Raslimali na Madeni.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha Maafisa Waandamizi wa jeshi la Polisi kutoka Mikoa mitatu ya Unguja. Mkoa wa Mjini, Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kusini Unguja.



*Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar CP Hamad Khamis Hamad akiongea na maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi katika semina ya mafunzo ya Maadili kwa Viongozi wa Umma tarehe 29 Novemba 2023.*

# SIMBACHAWENE: TUJIKITE KUZUIA RUSHWA BADALA YA KUPAMBANA MADHARA YAKE

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amezitaka taasisi zinazohusika na kusimamia utawala bora nchini, kujikita Zaidi katika kuzuia vitendo vya rushwa hususani kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo badala ya kusubiria mpaka rushwa itokee ndipo wanaanza kupambana nayo.

"Wakati mwingine tunaweka nguvu kubwa na rasilimali nyingi katika kupambana na rushwa wakati ambapo matokeo ya rushwa yanakua tayari yameshatokea na kuleta madhara kwa serikali badala yake tulipaswa kutumia nguvu hiyo hiyo katika kuzuia rushwa isiweze kutokea" alisema.

Mhe. Simbachawene alisema hayo kwenye kongamano la jukwaa la kitaifa la wadau wa juhudi dhidi ya rushwa lililofanyika tarehe 04 Desemba , 2023 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya maadili na haki za binadamu nchini ambapo kilele chake ni tarehe 10 Desemba,2023. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni "Zingatia Maadili, Utu, Uhuru, na Haki kwa watu wote kwa maendeleo endelevu"




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb) akiongea na wana kongamano (hawapo pichani) la jukwaa la kitaifa la wadau wa juhudi dhidi ya rushwa lililofanyika tarehe 04 Desemba, 2023 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya Maadili na Haki za Binadamu nchini ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 10 Desemba,2023.*

Katika hotuba yake Mhe. Simbachawene alibainisha kuwa kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini ikiwemo tafiti kuhusu hali ya ya Utawala Bora nchini zimebaini kuwa rushwa ni mojawapo ya changamoto katika ufikiwaji wa lengo la serikali la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya, miundombinu, maji na nk.

"Niwahakikishieni Serikali yetu haitaacha kukabiliana na vitendo vya rushwa na kupambana inapobidi kwa kuwa zipo njia mbalimbali za kuzuia rushwa isiweze kutokea mojawapo ni hii ya kujadili pamoja mbinu za kuboresha zaidi usimamizi wa miradi ya maendeleo" alisema.

Katika hatua nyingine Mhe. Simbachawene alieleza kuwa matarajio ya Serikali kupitia mdahalo huo ni kupata mbinu mpya na mawazo mapya ya namna ya kuweza kupambana na rushwa ili kuweza kukuza Maadili nchini .

"Ni Imani yangu kuwa wadau wa sekta zote kwa umoja wetu tutatenda haki kwa mada zitakazowasilisha kwenye jukwaa ili kuweza kutoka na maazimio yatakayosaidia juhudi za kuzuia Rushwa badala ya kusubiri na kupambana wakati tumeshapoteza rasilimali nyingi" alisema.

Awali akitoa neno la utangulizi Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ambaepia ni mwenyekiti wa maadhimisho hayo Mhe. Jaji (Mst) Sivangilwa Mwagesi alisema kuwa

moja kati ya shughuli zilizopanga kutekelezwa katika maadhimisho ya mwaka huu ni Jukwaa la kitaifa la Wadau wa Juhudi ya Rushwa ambalo linakutanisha wadau mbalimbali kutoka Taasisi za Umma watakao jadili kwa kina kuhusu uadilifu wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Jaji (Mst) Sivangilwa Mwagesi alieleza kuwa kila tarehe 10 desemba, Tanzania huungana na nchi nyingine Duniani kuadhimisha siku ya Haki za Binadamu Kimataifa ambalo chimbuko lake ni tamko la Haki za Binadamu lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, tarehe 10 Desemba, 1948 (Universal Declaration of Human Rights - UDHR).

Siku ya Maadili na Haki za Binadamu hapa nchini ilianza kuadhimishwa kwa pamoja mwaka 2016 ikiwa ni muunganiko wa siku mbili yaani siku ya Maadili na Haki za Binadamu.

Maadhimisho hayo huratibiwa na taasisi zinazosimamia utawala bora ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wizara ya Katiba na Sheria, Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Utumishi wa Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

**Scan kusoma Jarida kidijitali**



*Baadhi ya Viongozi kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakifuatilia jukwaa la kitaifa la wadau wa rushwa lililofanyika tarehe 04 Desemba,2023 katika ukumbi wa PSSSF Jijini Dodoma. Wa kwanza kushoto ni Katibu Idara ya Ukuzaji Maadili Bw, Waziri Kipacha, wa tatu kushoto ni Katibu Idara ya Usimamizi Maadili Bw. John Kaole na kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu Bi. Teddy Njau.*



*Baadhi ya Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioshiriki kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamiu Kitaifa katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 10 Desemba, 2023*



*Wanachama wa klabu ya Maadili ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya msingi Chadulu jijini Dodoma, Mwanyama Boniface na Brown Liberty pamoja na mlezi wa klabu hiyo Mwalimu Jaquiline Chaula wakishiriki zoezi la upandaji miti shuleni hapo. Zoezi hilo lililoandaliwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kanda ya Kati- Dodoma tarehe 23 Januari, 2024.*



*Bw. Amon Sembiga, Mwalimu Mkuu wa Shule ya msingi Makulu jijini Dodoma, akiwaongoza wanafunzi wa Klabu ya Maadili kupanda miti iliyotolewa na Ofisi Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati Dodoma. Katiati ya wanafunzi ni Bi Jasmin Awadhi (mwenye kitambaa cheusi), Katibu Msaidizi, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili wa Umma akishuhudia zoezi la upandaji miti tarehe 19 Januari 2024.*

# VIONGOZI WA UMMA WATAKIWA KUJIEPUSHA NA MGONGANO WA MASLAHI

Mkuu wa Wilaya ya Muleba Mkoani Kagera Dkt. Abel Nyamahanga amewataka Viongozi wa Umma kuviishi viapo walivyo apa kikiwemo kiapo cha Ahadi ya Uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao na kuepukana na vitendo vya mgongano wa maslahi ili kujenga imani ya wananchi wanaowaongoza.

Dkt. Nyamahanga ametoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya Viongozi wa Umma kuhusu Maadili yaliyoendeshwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba tarehe 23 Januari, 2024.

"Serikali inatumia fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo kupitia katika halmashauri mbalimbali nchini hivyo, rasilimali hizo zinahitaji usimamizi mzuri wa Viongozi,v" amesema.

Dkt. Nyamahanga ameongeza kuwa Viongozi wa Umma wanayo dhamana kubwa katika kusimamia rasilimali za umma kwa umakini na uadilifu mkubwa ili kujenga imani kwa wananchi wanaowaongoza.

Amewataka viongozi kuzingatia maelekezo ya Serikali katika utendaji wa kazi kwa kufanya maamuzi sahihi kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Awali akieleza lengo la mafunzo hayo Katibu Msaidizi Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Bw. Godson Kweka ni kuwakumbusha viongozi wa umma nchini kuelewa dhana ya uwajibikaji wa pamoja.



*Mkuu wa Wilaya ya Muleba Dkt. Abel Nyamahanga akifungua mafunzo ya maadili ya viongozi wa Umma yaliyo fanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba tarehe 23 Januari 2024.*

Bw. Kweka aliendelea kuwakumbusha Viongozi hao kujiepusha na vitendo vyote vinavyopelekea uwepo wa mgogoro wa maslahi na kuwataka Viongozi hao kufanya kazi kwa uadilifu na uaminifu mkubwa ili kujenga imani kwa wananchi wanaowaongoza.

Bw. Kweka pia amewataka viongozi kusimamia rasilimali za umma kwa uadilifu mkubwa hasa pesa za miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmashauri.

Kuhusu urejeshaji wa Tamko la Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma kwa mwaka jana 2023 amesema asilimia 90 ya Viongozi wote wa Halmashauri ya Muleba walirejesh Matamko yao kwa wakati.

Aidha mafunzo hayo ya Maadili ya Viongozi wa Umma yamehudhuriwa na Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba zaidi ya 100 kutoka katika Idara, Vitengo pamoja na waheshimiwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo.



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya maadili wakisikiliza kwa makini mada zinazotolewa katika ukumbi wa Halmashauri ya Muleba yaliyofanyika tarehe 23 Januari 2024.*



*Bw. Anno Mgane, Afisa kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma akiongea na wanachama wa Klabu ya Maadili wa Shule ya Sekondari Ngh'onganha jijini Dodoma tarehe 18.1.2024 kabla ya zoezi la kupanda miti ili kuhifadhi mazingira ya shule hiyo. Miti hiyo imetolewa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati Dodoma. Ofisi imepanga kupanda miti 3,000 mwaka huu katika mikoa ya Dodoma na Singida ili kutunza mazingira.*



*Wanachama wa klabu ya Maadili ambao ni Wanafunzi wa shule ya Sekondari Ngh'onganha iliyopo jijini Dodoma wakipanda miti iliyotolewa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati. Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kati imepanga kutoa miche ya miti kwa shule 150 zenye Klabu za Maadili katika mikoa ya Dodoma na Singida ili kulinda mazingira.*

# WASILIANA NA OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

## MAKAO MAKUU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma
Makao Makuu, Ghorofa ya 7, Jengo la KAMBARAGE TOWER, 18 Br. Jakaya Kikwete S.L.P 225, DODOMA
ec@maadili.go.tz | +255 262160190 /+255262160192 | 022 2119217

## OFISI ZA KANDA

**Kanda ya Kati**
**Mikoa ya Dodoma na Singida**
S.L.P 1887 Dodoma,
Nanenane
Barua pepe : dodoma@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 26 232 1059

**Kanda ya Ziwa**
**Geita, Kagera, Mara na Mwanza Regions**
S.L.P 1473 Mwanza
Mt Kenyatta
Jengo la NSSF,
Barua pepe : mwanza@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 28 2505005

**Special Zone**
**Mikoa ya Dar ea Salaam, Pwani, Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba, Kusini Unguja**
Jengo la Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili, Mtaa wa Holand
S.L.P 13341,
Dar es Salaam,
Barua pepe : dsm@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 22211810

**Kanda ya Kaskazini**
**Mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro**
Jengo la Hazina
S.L.P 3174 Arusha,
Barua pepe : arusha@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 272970774

**Kanda ya Mashariki**
**Mikoa ya Morogoro na Tanga**
S.L.P 212 Morogoro,
Jengo la Mafao NSSF,
Barua pepe : morogoro@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 23 2613741

**Kanda ya Magharibi**
**Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Simiyu**
S.L.P 1126 Tabora,
Ofisi ya Kilimo, Br. Boma
Barua pepe : tabora@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 26 2605322

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHIF,
S.L.P 6311,
Mbeya.
Barua pepe : mbeya@maadILI.GO.TZ
Simu/Nukushi
Simu: Simu: +255 25 250 2714

**Kanda ya Kusini**
**Mikoa ya Lindi, Mtwara and Ruvuma**
S.L.P 218
Mtwara,
Mt. Chikongola , Barabara ya TANU
Barua pepe : mtwara@maadili.go.tz
Simu/Nukushi
Simu: +255 23 23233963

**Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipata maelezo kutoka kwa Bw. Waziri Kipacha Katibu Ukuzaji Maadili ya Viongozi wa Umma alipotembelea banda la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika viwanja vya Nyerere Square, Dodoma tarehe 10 Desemba, 2023. Anayeshuhudia katikati ni Mhe. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**



**Limeandaliwa na...**
**Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.**
**Makao Makuu, Ghorofa ya 7, Jengo la KAMBARAGE TOWER, 18 Br. Jakaya Kikwete S.L.P 225, DODOMA**
**ec@maadili.go.tz**
**+255 262160190 /+255262160192**
www.maadili.go.tz @sekretarieti ya maadili

**Scan kusoma Jarida kidijitali**